# JITAHIDI KULINGANISHA

## Kuwa mwumini kwa hiari

Gerhard Nehls

02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 1 01-11-2021 20:29:38

Original Title: Purpose & Aim

This is a publication of
Life Challenge © SIM 2021
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**info@lifechallenge.de**

All rights reserved. No part of this book may be reproduced without written permission, except for brief quotations in books and critical reviews.

Translation: John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania

Printed and bound in Kenya

02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 2 01-11-2021 20:29:38

# Jitahidi Kulinganisha

## JE, UTAKUBALIANA?

Lazima iwepo njia bora zaidi ya kuwasiliana kuliko kubadilishana hoja zilizotumiwa kwa werevu ambazo mara nyingi humchukiza sana mtu asiyeshikilia misimamo yake mwenyewe.

Waislamu na Wakristo wamekuwa katika kutokukubaliana kwenye baadhi ya masuala ya msingi. Madai kuhusu asili ya kimungu ya Vitabu vyao Vitakatifu na nafasi ya Yesu au Muhammad hukosolewa. Ni kawaida tu kuwa wafuasi wa kila imani watafute hoja na utetezi wa kusudi lao.

Wakristo hukanganywa kuhusu mashambulizi mengi ya kuumiza dhidi ya Kitabu chao kutokana na dhana fulani za Kiislamu kuhusu Yesu; na huwaomba kwa moyo safi Waislamu wasikie pia kuhusu upande mwingine wa simulizi.

Mtu mwaminifu na wa kiroho hatakubali tu mila zake mwenyewe na kuzifuata, lakini pia atausikiliza vema na upande ule mwingine. Ni wachache waliochukua muda na kufanya juhudi wakalinganisha kauli za Kurani na za Biblia kuhusu vitabu hivyo viwili au utu wa Yesu unavyoonyeshwa humo. Nukuu tulizokusanya ni chache tu, lakini tutajisikia kufaidika sana kutokana na juhudi zetu kama nukuu hizi zitawahamasisha wasomaji wetu kufanya uchunguzi wao kwa kulinganisha.

Kwa vyovyote: Jitahidi Kulinganisha!



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 1 01-11-2021 20:29:38

## INAVYOSEMA KURANI KUHUSU BIBLIA

"Semeni nyinyi: 'Tumemwamini Mwenyezi Mungu, na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu, na Ismaili, na Is-haqa, na Yaaqubu, na kizazi (chake Yaaqubu); na waliyopewa Musa, na Isa, na pia yale waliyopewa Manabii kutoka kwa Mola wao: HATUTAFAUTISHI BAINA YA YOYOTE KATIKA HAO."

(Sura al-Baqarah 2:136)

"Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye, - Mwenye uhai wa milele, (na) Mwendeshaji wa mambo yote. Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na Aliteremsha Taurati (ya Musa) na Injili (ya Isa) ... ziwe uwongozi kwa watu." (Sura Al-Imran 3:2-4)

"Enyi mlioamini! Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha juu ya Mtume Wake." (Sura an-Nisa 4:136)

"Hakika Tuliteremsha Taurati (kwa Musa); yenye uwongozi na nuru ... Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri ... Na Tukawafuatishia Isa, bin Maryamu, kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati: Tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongozi na nuru ... na uwongozi na mauidha kwa wamchao.

WATU WA INJILI WAHUKUMU KWA YALE ALIYOYATEREMSHA MWENYEZI MUNGU NDANI YAKE. NA WASIOHUKUMU KWA (kufuata) YALE ALIYOYATEREMSHA MWENNYEZI MUNGU BASI HAO NDIO WAASI.

Wahukumu ... kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao ..."

(Sura al-Maidah 5:44, 46, 47, 49)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 2 01-11-2021 20:29:38

> "Enyi watu wa 'Kitabu' ... msimamishe Taurati na Injili na haya yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa MOLA WENU." (Sura 5:68)

> "QuranI ... ni maelezo ya Vitabu (vilivyopita)." (Sura Yunus 10:37)

> "Na kama unayo shaka juu ya hayo Tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao Vitabu kabla yako. Kwa yakini haki imekwisha kukujia kutoka kwa Mola wako." (Sura 10:94)

> "WALA MSIBISHANE NA WATU WALIOPEWA KITABU ... NA SEMENI: TUNAAMINI YALIYOTEREMSHWA KWETU NA YALIYOTEREMSHWA KWENU." (Sura al-Ankabut 29:46)

> "Na hii (Qurani) ni kitabu Tulichokiteremsha, chenye baraka nyingi, kinahakikisha yale yaliyokitangulia: Na ili uwaonye (watu wa) Mama wa miji (Makka) na watu walio pembezoni mwake." (Sura al-Anam 6:92)

Hakika haya yanaweza kuwa na maana tu kuwa Muhammad alileta ufunuo Makka na kwa Waarabu, akiyathibitisha yale yaliyoletwa kabla yake.

> "Hatukuwatuma kabla yako ila wanaume Tuliowafunulia: BASI WAULIZENI WENYE KUMBUKUMBU ikiwa nyinyi hamjui." (Sura al-Anbiya 21:7)

Tunaweza kuona wazi kuwa Qurani humaanisha huo ufunuo wa Mungu wa "Kitabu" na yaliyomo ambayo yote hayakuchafuliwa wakati wa mtume Muhammad. Hata hivyo Qurani hukosoa kupotoshwa na kutafsiriwa vibaya kwake.

> "Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na mna ficha haki, hali mnajua?" (Sura Al-Imran 3:71)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 3 01-11-2021 20:29:38

> “Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); wala si ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu).”
>
> (Sura 3:78)

(Mikazo yote kwenye nukuu ni ya mwandishi.)

Kama kuna kinachoonekana wazi kabisa, ni kuwa Kurani hukazia kuwa Taurati na Injili ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Na Wakristo wanaamini hivyo. Kurani inaongeza:

> “Hakuna mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu.” (Sura Yunus 10:64)

> “Na hakuna abadilishaye maneno ya Mwenyezi Mungu.” (Sura al-Anam 6:34)

> “Na hatukumtuma kabla yako Mtume, … ila anaposoma, shetani hutia (fitina) katika masomo yake hayo. Lakini Mwenyezi Mungu huondoa anayoyatia shetani, kisha Mwenyezi Mungu huzimakinisha Aya Zake; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.”
>
> (Sura al-Hajj 22:52)

*Historia na elimukale* humzuia mtu asidai kuwa Biblia imekuwa na badiliko lolote.

Muhammad alipolenga “Kitabu” au “Taurati”, Zaburi” au “Injili”, bila shaka alilenga kitabu kilichokuwako Uarabuni siku zake na kizazi chake.

Kama maneno yana maana yote, basi Muhammad alikuwa akikilenga “Kitabu” (al-Kitab) hiki kuwa ndiyo yaliyoteremshwa.

Zaidi ya hayo, kwa nini Myahudi au Mkristo kabla au baada ya Muhammad atamani kuubadilisha ufunuo wa Mungu? Anataka aende motoni? – Huenda wengi hawalitambui onyo kali la mwishoni kabisa mwa Biblia:

> *“Namwonya kila mtu asikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki; Mtu ye yote akiongeza humo cho chote, Mungu*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 4 01-11-2021 20:29:38

*atamwongezea mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Kama mtu ye yote akipunguza humo cho chote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sheemu yake katika ule mti wa uzima na katiika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki."* (Ufunuo 22:18, 19)

Hizi ndizo aya za mwisho haswa kwenye Biblia. Sababu pekee ya kuanzisha mabadiliko inayoweza kujitokeza ni kuielezea tofauti kati ya Kurani na "Kitabu". Waislamu, wakiona kuwa "Kitabu" kinapingana na Kurani, hudai kuwa Biblia imepotoshwa.

Karne nne za mwanzo baada ya Muhammad (600-1000 BK) hakuna mwanatheolojia Mwislamu aliyedai kuwa vifungu vya Injili havikuwa vya kweli. Ilikuwa tu Ibn-Khazm, aliyekufa huko Cordoba mwaka wa 1064, ndipo ubatilishaji huu ulianza.

**Ilikuwa tu Ibn-Khazm, aliyekufa huko Cordoba mwaka wa 1064, ndipo ubatilishaji huu ulianza**

Akiutetea Uislamu dhidi ya Wakristo, Ibn-Khazm alikumbana na pingamizi kati ya Kurani na Injili. Mfano mmoja wa wazi ni kifungu cha Kurani kinachosema, 'hawakumwua wala hawakumsulubu' (Sura an-Nisa 4:157). Ibn Khazm alidai, 'Kwa kuwa Kurani lazima iwe inasema ukweli, vya uongo lazima viwe ni vifungu vya Injili vinavyopinga. Lakini Muhammad anatuambia tuiheshimu Injili. Kwa hiyo, andiko la sasa ni upotoshaji wa Wakristo.' Msingi wa ubishi wake haukuwa kwenye ukweli wa kihistoria, bali hasa kwenye maoni yake mwenyewe na kutaka kwake kuyalinda yaliyomo kwenye Kurani.

Kwa kweli hiyo ilionekana kuwa njia rahisi zaidi ya kuwashambulia wapinzani. 'Tukithibitisha ubatili wa vitabu vyao, wanazipoteza hoja wanazozitoa humo.' Hatimaye hili lilipelekea atoe kauli hii: 'Wakristo waliipoteza Injili iliyofunuliwa isipokuwa viashirio vichache alivyoacha Mungu ili viwapinge.'



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 5 01-11-2021 20:29:38

Wasomi wengi mashuhuri wa Kiislamu wameukubali uhalisi wa andiko la Agano Jipya.

Ushuhuda wao huthibitisha kuwa mahojiano ya Wakristo na Waislamu hayapaswi kuzuiwa daima kwa madai yaliyoanzishwa na Ibn-Khazm. Wanahistoria wawili maarufu, Al-Mas'udi (aliyekufa mwaka wa 956) na Ibn-Khaldun (aliyekufa mwaka wa 1406), waliukubali uhalisi wa andiko la Injili. Wanatheolojia wanne maarufu sana walikubaliana na hili: Ali at-Tabari (aliyekufa mwaka wa 855), Qasim al-Khasani (aliyekufa mwaka wa 860), 'Amr al-Ghakhiz (aliyekufa mwaka wa 869) na wa mwisho ni, Al-Ghazzali (aliyekufa mwaka wa 1111). Mtazamo wao anao pia Abu Ali Husain Ibn Sina, anayejulikana huko Magharibi kama Avicenna (aliyekufa mwaka wa 1037); Al-Bukhari (aliyekufa mwaka wa 870), aliyejipatia sifa kubwa kwa kukusanya mapokeo ya asili, aliinukuu Kurani yenyewe (Sura al-Imran 3:72, 78) kuthibitisha kuwa andiko la Biblia halikupotoshwa. (Kulingana na kitabu cha Hans Wijngaard kinachoitwa "Can We Trust the Gospel?" yaani Tunaweza Kuiamini Injili?).

## ISEMAVYO KURANI KUHUSU YESU

1. **Alizaliwa na bikira** (Sura Maryam 19:16-35). Tazama anavyosema Mwenyezi Mungu: "Haya ni sahali Kwangu". (v.21) Bila shaka hili linaonyesha u Baba wa Mwenyezi Mungu. (Tafadhali, si kwa njia ya kimwili!) Hii ndiyo hasa imani ya Kikristo ya Mungu kuwa Baba wa Yesu Kristo.
2. **Alikuwa ndiye Masihi** (Sura an-Nisa 4:171). Kurani haiifafanui maana ya neno Masihi. Kwa hiyo lazima tusadiki kuwa maana ya kibiblia inakubaliwa. Utendaji wa Masihi uliotabiriwa na kupokelewa ni ule wa mkombozi kutoka dhambini.
3. **Alikuwa Roho iliyotoka kwa Mungu** (Sura an-Nisa 4: 171).
4. **Alikuwa Neno la Mungu** (Sura an-Nisa 4:171). Hili linaweza pia kuwa na maana ya "udhihirisho wa Mungu". Hili tena



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 6 01-11-2021 20:29:38

linakubaliana kabisa na Biblia (Yohana 1:1-14, Wakolosai 1:15).

5. **Hakuwa na dhambi** (Tafsiri ya Saleh Farsy), yaani alikuwa mtakatifu (Sura Maryam 19:19). Haya yalisemwa ili kutofautisha na mwanadamu au nabii mwingine ye yote.
   **Adamu** alitenda dhambi (Sura al-Baqarah 2:36, 7:22, 23).
   **Ibrahimu** alitenda dhambi (Sura al-Shu'ara 26:82).
   **Musa** alitenda dhambi (Sura al-Qasas 28:15, 16).
   **Yunus** alitenda dhambi (Sura as-Saffat 37:142).
   **Daudi** alitenda dhambi (Sura Sad 38:24, 25).
6. **Ni Mwenye hishima katika dunia na Akhera** (Sura Al-Imran 3:45).
7. **Alichukuliwa na Mungu hadi mbinguni** (Sura an-Nisa 4: 158).
8. **Atarudi duniani siku ya Kiyama** (Sura az-Zukhruf 43:61 tafsiri ya Yusuf Ali na Mishkat 4, uk.78-80).

*Kwa kuzingatia kauli hizi tu, kuna ye yote anaweza kudai kuwa Yesu alikuwa mwanadamu au nabii wa kawaida? Je, ni nabii yupi mwenye ubora na sifa kama hizi?*

## ISEMAVYO BIBLIA KUHUSU YESU

Uliwahi kutambua kuwa jina "Yesu" lina maana? Jina hili lina umuhimu mkubwa, maana siyo tu lilitabiriwa kwenye Taurati, bali pia lilitolewa kwa Mariamu na malaika Gabrieli. Yesu ni namna ya Kiswahili ya neno la Kiebrania "Yeshuah", na hilo lina maana ya "Wokovu." Kukataa kuwa Yesu si wokovu wetu ni kumkana Yesu kabisa, maana tukiona kuwa ana upungufu hatumheshimu. Agano la Kale, ambalo liliandikwa kati ya mwaka wa 1500 hadi 400 KK, lilitabiri au kutoa unabii wa kuja kwa Yeshuah (Yesu), huyo Masihi, kwenye vifungu vingi. Agano Jipya ambalo ni maandiko ya maisha na mafundisho ya Yesu, huuthibitisha kikamilifu unabii huu.

Wokovu huu kwa njia ya Yesu ambaye ndiye Masihi, umewasilishwa vema kwenye Injili. Kati ya sura 89 za Injili, 27

huzungumzia wiki ya mwisho ya maisha ya Yesu. Ili kuthibitisha ukweli huu lazima tuangalie ushahidi uliopo.

***Taarifa za Walioshuhudia***

Matukio haya hayakutokea mafichoni bila ya mashahidi wo wote. Yalitokea hadharani na Waisraeli wote waliyatambua. Injili ilipoandikwa na hao waandishi wanne, kama ulikuwa ni uongo Waisraeli wote wangesimama kuyapinga hayo. Kinyume chake, Mitume mara nyingi waliwahamasisha watu wawahoji wale walioshuhudia kwa macho yao. Paulo akijitetea mbele ya Mfalme Agripa alisema:

**Kuukataa ukweli kuwa Yesu ni Mwokozi wetu ni kumkataa Yesu mwenyewe, maana tukimpunguzia sifa yake tunamdharau**

*... Nanena kweli. ... Naam, Mfalme anajua kuhusu mambo haya yote, nami nasema naye kwa uhuru. Kwa sababu nina hakika kwamba hakuna hata mojawapo ya mambo haya asilolijua, kwa kuwa hayakufanyika mafichoni.*
(Matendo 26:25, 26)

Na Petro Siku ya Pentekoste wiki chache baada ya Yesu kusulibiwa, aliuambia mkutano mkubwa wa Wayahudi:

*Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa Nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo Mungu alitenda miongoni mwenu kupitia kwake, kama ninyi wenyewe mjuavyo.*

*Huyu mtu* [Yesu] *akiisha kutolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi, kwa mikono ya watu wabaya, mlimuua kwa kumgongomea msalabani. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeye kushikiliwa na nguvu za mauti.*
(Matendo 2:22-24)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 8 01-11-2021 20:29:38

Tunaona kuwa Wayahudi hawakukanusha kuuawa kwa Yesu msalabani. Walikanusha u Masihi wake na kufufuka kwake.

Baadaye kidogo Petro na baadhi ya Mitume wengine walitiwa gerezani kwa fundisho lao. Walipokuwa wakihojiwa na baraza la Wayahudi, walijibu:

> *Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, ambaye ninyi mlimuua kwa kumtundika kwenye msalaba. Mungu alimtukuza, akamweka mkono wake wa kuume kuwa Kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli toba na msamaha wa dhambi. Nasi tu mashahidi wa mambo haya, vivyo hivyo na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wale wanaomtii.* (Matendo 5:29b-32)

Paulo naye alisisitiza kuwa: ni *kama yasemayo Maandiko* (yaani unabii katika Torati) na kushuhudiwa na mashahidi wengi, ambao baadhi yao wakati huo walikuwa hai ili waweze kuulizwa. Haya yalisemwa kwenye waraka kwa watu wa Ugiriki, maana huko Israeli haikuwako haja ya kuyatamka maana waliyajua:

> *Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemavyo Maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuliwa siku ya tatu, kama yasemavyo Maandiko, na kwamba alimtokea Kefa* [yaani Petro]*, kisha akawatokea wale kumi na wawili. Baadaye akawatokea wale ndugu waumini zaidi ya 500 kwa pamoja, ambao wengi wao bado wako hai, ingawa wengine wamelala. Ndipo akamtokea Yakobo na kisha mitume wote.*
> (1 Wakorintho 15:3-7)

Hili tena linaungwa mkono na Mtume Petro kabla tu ya kuuawa kwake, akiikazia taarifa aliyoishuhudia kwa macho kwa kuonyesha unabii uliotimizwa kama ulio “hakika zaidi”. Shahidi anaweza kusema uongo. Hata mashahidi wengi wanaweza. Lakini katika unabii na kutimizwa kwake haiwezekani kuwamo uongo!



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 9 01-11-2021 20:29:38

*Tulipowafahamisha juu ya uweza na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo, hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, bali tulishuhudia kwa macho yetu ukuu wake. Alipewa heshima na utukufu kutoka kwa Mungu Baba, sauti ilipomjia katika Utukufu Mkuu, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa naye sana." Sisi wenyewe tuliisikia sauti hii ambayo ilitoka mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja naye kwenye ule mlima mtakatifu.*

*Nasi tunalo pia neno la hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vyema mkiliangalia kwa bidii, kama vile nuru inavyong'aa gizani, hadi kupambazuka na nyota ya asubuhi izuke mioyoni mwenu. Zaidi ya yote, yawapasa mjue kwamba hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa kama alivyopenda nabii mwenyewe. Kwa maana unabii haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.* (2 Petro 1:16-21)

### *Historia Inathibitisha Injili*

Sote tunajua ya kuwa kumbukumbu za kale za historia huzungumzia sana vita, mashujaa, na viongozi wa nyakati zile. Matukio ya maeneo yasiyojulikana kama vile Galilaya na Uyahudi ni nadra sana yatajwe. Hata yakitajwa, matukio ya kipaumbele yatahusu vita na falme. Hata hivyo, kuna ushahidi unaounga mkono kumbukumbu za Kibiblia.

**Cornelius Tacitus** alikuwa mwanahistoria maarufu sana wa enzi ya Kirumi. Anaelezea jinsi Wakristo walivyochukiwa na watu wengi kwa "makosa" yao na walivyosingiziwa ili waadhibiwe kwa moto na Warumi aliouanzisha Nero mwaka wa 64 BK. Anaandika:

> "Jina Mkristo huja kwao kutoka kwa Kristo, aliyeuawa na Pontio Pilato kwenye utawala wa Tiberio; na mazingaombwe hayo yenye madhara, yakakomeshwa kwa muda, yalivuma upya na kuenea siyo tu katika Uyahudi yalikoanzia maradhi haya, bali hata katika



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 10 01-11-2021 20:29:38

> Rumi yenyewe, ambako kila jambo la aibu huja na kuhusudiwa."

Ni wazi kuwa Tacitus hakuwa na huruma kwa Ukristo: Dini ilioyonwa kuwa ni ya watu wa hali ya chini, na hasa watu wa mashariki. Kwa hiyo ushahidi wake ni muhimu zaidi.

**Josephus** alikuwa mmoja wa viongozi wa Kiyahudi aliyehusika na upinzani dhidi ya Warumi mwaka wa 70 BK. Aliandika kwenye kitabu chake "Antiquitates iudaicae" cha mwaka wa 93 BK na "De bello iudaicae" cha mwaka wa 75-79 BK kuueleza umma wa Warumi kuhusu dini ya baba zake ... Katika haya tunakutana na watu wengi tunaowajua kutoka kwenye Agano Jipya: Pilato, Annas, Caiaphas, Herod, Cyrenius, Felix, Festus na wengine. Anaandika pia kuhusu Yohana Mbatizaji, kuhubiri kwake, kubatiza kwake na kuuawa kwake. Hata hivyo la muhimu zaidi ni pale anapomtaja Yesu mwenyewe.

> "Sasa kwenye nyakati hizi alikuwako Yesu, mtu mwenye hekima, kama inafaa kumwita yeye kuwa ni mtu, maana alikuwa akitenda matendo makuu ya ajabu, mwalimu wa watu wanaoipokea kweli kwa furaha. Aliwavutia wengi, Wayahudi na watu wa Mataifa. Ndiye aliyekuwa Kristo (Masihi). Na Pilato akikubali pendekezo la wakuu kati yetu, alipokuwa amemhukumu kifo cha msalabani, waliompenda mwanzoni, hawakumwacha; maana siku ya tatu aliwatokea tena akiwa hai; maana manabii wa Mungu walikuwa wameyatabiri haya na mambo mengine elfu kumi kuhusu huyu Yesu Kristo. Na kabila la Wakristo, kama walivyoitwa kutokana na yeye, lipo hadi leo."
>
> ("Antiquitates iudaicae", Vol. 18,111:3)

### *Unabii Uliotimia Huithibitisha Injili*

Sote tunajua kuhusu miujiza ya Yesu. Lakini kwenye "Mishkat", Al-Haj Maulana Fazlul Karim anatamka kwa usahihi hivi:

> "Jambo kuu katika miujiza ni unabii, yaani kutabiri matukio yajayo. Huu si utabiri wa kisiasa bali ni utabiri wa siri zijazo zinazotoka kwenye ufahamu wa Mungu. Unabii ni mkuu



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 11 01-11-2021 20:29:38

kuliko muujiza kwa sababu zifuatazo. Unabii unaweza kuthibitishwa kihistoria lakini muujiza hauwezi. Unabii hudhihirisha kufahamu kabla kwa Mungu, na muujiza hudhihirisha uwezo wa Mungu. Kwa kuwa ufahamu ni mkuu kuliko uwezo, unabii ni mkuu kuliko muujiza."

Kwenye Injili Iliyoandikwa na Mathayo kuna unabii zaidi ya 60 za uliotimia! Kwenye orodha, (kutoka kwa wanafunzi wengine wa Yesu) inathibitisha jambo hili.

**Unabii wa mahali atakapozaliwa Yesu na kuwapo kwake hata kabla ya kuzaliwa kimwili, mwaka wa 700 KK:**

*"Lakini wewe, Bethlehemu Efrathi, ingawa u mdogo miongoni mwa koo za Yuda, kutoka kwako atatokea kwa ajili yangu yeye atakayekuwa mtawala katika Israeli, ambaye asili yake ni kutoka zamani, kutoka milele."*

(Mika 5:2)

**Kutimia:**

*Hivyo Yosefu akapanda kutoka mji wa Nazareti ulioko Galilaya kwenda Uyahudi, mpaka Bethlehemu, mji wa Daudi, kwa sababu yeye alikuwa wa ukoo na wa nyumba ya Daudi. Alikwenda huko kujiandikisha pamoja na Maria, ambaye alikuwa amemposa naye alikuwa mjamzito. Wakiwa Bethlehemu, wakati wa Maria wa kujifungua ukawa umetimia, naye akamzaa mwanawe, kifungua mimba. Akamfunika nguo za kitoto na kumlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni.* (Luka 2:4-7)

**Unabii wa kuzaliwa na bikira, uungu na uwana wa kipekee wa Yesu mwaka wa 700 KK:**

*Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara: Bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana, na ataitwa Imanueli.* [Mungu pamoja nasi] (Isaya 7:14)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 12 01-11-2021 20:29:38

*Kwa maana, kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanaume, nao utawala utakuwa mabegani mwake. Naye ataitwa Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani.* (Isaya 9:6)

**Kutimia:**

*Basi Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Maria mama yake alikuwa ameposwa na Yosefu, lakini kabla hawajakutana kimwili, Maria alionekana kuwa na mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa Yosefu, mwanaume aliyekuwa amemposa alikuwa mtu mwadilifu, hakutaka kumwaibisha Maria hadharani, aliazimu kumwacha kwa siri.*

*Lakini mara alipoazimu kufanya jambo hili, malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto na kusema, "Yosefu mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Maria awe mke wako, kwa maana mimba aliyo nayo ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atamzaa mwana, nawe utamwita Jina lake Yesu, kwa maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao."*

*Haya yote yalitukia ili litimie lile Bwana alilokuwa amenena kupitia nabii, akisema: "Tazama, bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana, nao watamwita Jina lake Imanueli": maana yake, "Mungu pamoja nasi."* (Mathayo 1:18-23)

Hili limethibitishwa na vifungu vingi katika Kurani.

**Unabii kuhusu kuja kwa Yesu ulitolewa na nabii Danieli 9:24 mwaka wa 500 KK:**

Kifungu hiki kina mambo mchanganyiko mno kutumiwa kwenye kijitabu cha aina hii. Msomaji anayependa anaweza kupata maelezo zaidi kwa kuandika akitumia anwani iliyotolewa mwishoni mwa kijitabu hiki.



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 13 01-11-2021 20:29:38

**Unabii unaotabiri kuwa Yesu alikuja kuokoa na kuponya, mwaka wa 700 KK:**

> *... tazama, Mungu wenu atakuja, pamoja na malipo ya Mungu, atakuja na kuwaokoa ninyi. Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa na masikio ya viziwi yatazibuliwa.*
> (Isaya 35:4, 5)

**Kutimia:**

**A. Alikuja kuokoa.**

> *"Naye atamzaa mwana, nawe utamwita Jina lake Yesu, kwa maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao."* (Mathayo 1:21).

> *"Kwa maana Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."* (Luka 19:10)

> *"Hakuna mtu yeyote aliyekwenda mbinguni isipokuwa yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu. Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu. Ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele.*
>
> *Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kupitia kwake ulimwengu upate kuokolewa. Yeyote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Kwa kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe. Lakini yule aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru, ili ionekane wazi kwamba matendo yake yametendeka katika Mungu."*
> (Yohana 3:13-21)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 14 01-11-2021 20:29:38

*Lakini sasa, haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa pasipo sheria, ambayo Sheria na Manabii wanaishuhudia. Haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo kwa wote wamwaminio. Kwa maana hapo hakuna tofauti, kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu. Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki yake, kwa sababu kwa ustahimili wake aliziachilia zile dhambi zilizotangulia kufanywa. Alifanya hivyo ili kuonyesha haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu.* (Warumi 3:21-26)

*Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa kupitia kwake tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo ndani yake sasa tunasimama, nasi twafurahia katika tumaini letu la kushiriki utukufu wa Mungu.* (Warumi 5:1-2)

*Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu ... Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima katika Kristo Yesu imeniweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti.* (Warumi 8:1-2)

**B. Alikuja kuponya.**

*Yesu akasimama, akawaamuru wamlete huyo mtu kwake. Alipokaribia, Yesu akamuuliza, "Unataka nikufanyie nini?" Akajibu, "Bwana, nataka kuona." Yesu akamwambia, "Basi upate kuona. Imani yako imekuponya." Akapata kuona saa ile ile, akamfuata Yesu, huku akimsifu Mungu. Watu wote walipoona mambo hayo, nao wakamsifu Mungu.* (Luka 18:40-43)

*Yesu akapita katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri habari njema za Ufalme, na*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 15 01-11-2021 20:29:38

*akiponya kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni mwa watu. Kwa hiyo sifa zake zikaenea sehemu zote za Shamu, nao watu wakamletea wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali na maumivu, waliopagawa na pepo wachafu, wenye kifafa na waliopooza, naye akawaponya.* (Mathayo 4:23-24)

*Yohana* [Mbatizaji] *aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo Kristo alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi wake ili wakamuulize, "Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?" Yesu akajibu, "Rudini mkamwambie Yohana yale mnayosikia na kuyaona: Vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa na mimi."* (Mathayo 11:2-6)

*Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagawa na pepo wachafu, naye akawatoa wale pepo wachafu kwa neno lake, na kuwaponya wagonjwa wote. Haya yalifanyika ili litimie lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya kwamba: "Mwenyewe alitwaa udhaifu wetu na alichukua magonjwa yetu."* (Mathayo 8:16-17)

*Kisha mtu mmoja, jina lake Yairo, aliyekuwa kiongozi wa sinagogi, akaja na kuanguka miguuni mwa Yesu, akimwomba afike nyumbani kwake, kwa kuwa binti yake wa pekee, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa anakufa.. . . akaja mtumishi kutoka nyumbani kwa Yairo, yule kiongozi wa sinagogi, kumwambia, "Binti yako amekwisha kufa. Usiendelee kumsumbua Mwalimu."*

*Yesu aliposikia jambo hili, akamwambia Yairo, "Usiogope. Amini tu, naye binti yako atapona."*

*Walipofika nyumbani kwa Yairo . . . wote walikuwa wakilia na kuomboleza kwa ajili ya huyo binti. Yesu akawaambia, "Acheni kulia. Huyu binti hajafa, ila amelala."*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 16 01-11-2021 20:29:38

*Wao wakamcheka kwa dharau, wakijua kuwa amekwisha kufa. Yesu akamshika yule binti mkono na kuita, "Binti, amka!" Roho yake ikamrudia, naye akainuka mara moja.*
(Luka 8:41-55; ona pia Luka 7:1-10)

**Unabii unaolitabiri jina la Yesu - mwaka wa 700 KK:**

*Nisikilizeni, enyi visiwa, sikieni hili, ninyi mataifa mlio mbali: Kabla sijazaliwa, BWANA aliniita, tangu kuzaliwa kwangu, amelitaja jina langu. Akafanya kinywa changu kuwa kama upanga ulionolewa ... Pia nitakufanya uwe nuru kwa ajili ya watu wa Mataifa,ili upate kuleta* ***wokovu*** *wangu* [Kiebrania yaani Yeshuah, jina halisi la Yesu, alipoishi Israeli] *hata miisho ya dunia." Hili ndilo asemalo BWANA, yeye Mkombozi na Aliye Mtakatifu wa Israeli, kwake yeye aliyedharauliwa na kuchukiwa na taifa ...*
(Isaya 49:1-7; Tazama pia Isaya 12:2-3 ukizingatia Yohana 7:37, 4:10-14, Ufunuo 21:6, Isaya 52:10, etc.)

Kutimia**:**

**Malaika alimwambia Yusufu:**

*"Naye* [Mariamu] *atamzaa mwana, nawe utamwita Jina lake Yesu, kwa maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao."* (Mathayo 1:21)

Hadi hapa Waislamu na Wakristo kwa kiasi fulani wanakubaliana, ingawa Waislamu wanaweza kukipinga kifungu cha Isaya kinachotabiri au kutamka uungu na u Mwana wa Yesu. Lakini lazima tuangalie uzito wa dai lake kuwa ni Mungu kwenye unabii na kutimia kwake.

Kumbuka: Hakuna mtu mwingine anayeweza kusemwa kuwa

1. Alizaliwa kimiujiza hivyo
2. Aliponya magonjwa yote na kufufua wafu
3. Alitoa pepo wachafu
4. Hakuwa na dhambi, alikuwa mtakatifu ... (Sura 19:19; Waebrania 4:15; 1 Yohana 3:5; 2 Wakorintho 5:21; 1 Petro 2:22; Isaya 53:9; nk.)

5. Yeye ni Neno la Mungu ... (Sura 4:171, Yohana 1:1-2, 14)
6. Yeye ni Roho itokayo kwa Mungu ... (Sura 4:171)
7. Maisha yake yametabiriwa kwa kina mamia ya miaka kabla ya kutimia kwake.

Sasa tuuangalie mwisho wa maisha ya Yesu kama ulivyotabiriwa katika Agano la Kale, na kutimia kwake.

**Unabii wa Yesu kuingia Yerusalemu kwa unyenyekevu akiwa amepanda Punda - mwaka wa 480 KK:**

> *Shangilia sana, ee Binti Sayuni! Piga kelele, Binti Yerusalemu! Tazama, Mfalme wako anakuja kwako, ni mwenye haki, naye na wokovu, ni mpole, naye amepanda punda, mwana-punda, mtoto wa punda.* (Zekaria 9:9)

Kutimia**:**

> *Walipokaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage katika Mlima wa Mizeituni. Ndipo Yesu akawatuma wanafunzi wake wawili, akawaambia, "Nendeni katika kijiji kilichoko mbele yenu, nanyi mtamkuta punda amefungwa hapo, na mwana-punda pamoja naye. Wafungueni na mniletee. Kama mtu yeyote akiwasemesha lolote, mwambieni kwamba Bwana ana haja nao, naye atawaruhusu mwalete mara."*
>
> *Haya yalitukia ili litimie lile lililonenwa na nabii, akisema: "Mwambieni Binti Sayuni, 'Tazama, mfalme wako anakuja kwako, ni mnyenyekevu, naye amepanda punda, juu ya mwana-punda, mtoto wa punda.' "*
>
> *Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya kama Yesu alivyokuwa amewaagiza. Wakamleta yule punda na mwana-punda, nao wakatandika mavazi yao juu ya hao punda, naye Yesu akaketi juu yake. Umati mkubwa wa watu ukatandaza mavazi yao barabarani, na wengine wakakata matawi kutoka kwenye miti, wakayatandaza barabarani. Ule umati wa watu uliomtangulia na ule uliomfuata ukapiga kelele ukisema, "Hosana, Mwana wa*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 18 01-11-2021 20:29:38

*Daudi!" "Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la Bwana!" "Hosana juu mbinguni!"* (Mathayo 21:1-9)

**Unabii wa Yesu kusalitiwa - mwaka wa 480 KK:**

*Hata rafiki yangu wa karibu niliyemwamini, ... ameniinulia kisigino chake.* (Zaburi 41:9)

*Nikawaambia, "Mkiona kuwa ni vyema, nipeni ujira wangu, la sivyo, basi msinipe." Kwa hiyo wakanilipa vipande thelathini vya fedha. Naye BWANA akaniambia, "Mtupie mfinyanzi," hiyo bei nzuri waliyonithaminia! Kwa hiyo nikachukua hivyo vipande thelathini vya fedha na kumtupia huyo mfinyanzi katika nyumba ya Bwana.* (Zekaria 11:12-13)

Kutimia**:**

*Kisha Yuda Iskariote, mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili, akaenda kwa viongozi wa makuhani ili kumsaliti Yesu kwao. Walifurahi sana kusikia jambo hili na wakaahidi kumpa fedha. Hivyo yeye akawa anatafuta wakati uliofaa wa kumsaliti.* (Marko 14:10-11)

*Ilipofika jioni, Yesu akaja pamoja na wale wanafunzi wake kumi na wawili. Walipoketi mezani wakila, Yesu akawaambia, "Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti, mmoja anayekula pamoja nami."*

*Wakaanza kuhuzunika na kumuuliza mmoja baada ya mwingine, "Je, ni mimi Bwana?" Akawajibu, "Ni mmoja miongoni mwenu ninyi kumi na wawili, yule anayechovya mkate kwenye bakuli pamoja nami. Mwana wa Adamu anaenda zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini ole wake mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu huyo kama hangezaliwa.* (Marko 14:17-21)

*Yuda, mmoja wa wale wanafunzi Kumi na Wawili, akatokea. Alikuwa amefuatana na umati wa watu wenye panga na marungu, waliokuwa wametumwa na viongozi*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 19 01-11-2021 20:29:38

*wa makuhani, walimu wa sheria, na wazee. Basi msaliti alikuwa amewapa hao watu ishara, kwamba: "Yule nitakayembusu ndiye. Mkamateni, mkamchukue chini ya ulinzi." Mara Yuda akamjia Yesu na kusema, "Rabi." Akambusu. Wale watu wakamkamata Yesu, wakamweka chini ya ulinzi.* (Marko 14:43-46)

*Yuda, ambaye alikuwa amemsaliti Yesu, alipoona kuwa Yesu amehukumiwa, akajuta na akarudisha vile vipande thelathini vya fedha alivyopewa na viongozi wa makuhani na wazee wa watu. Akasema, "Nimetenda dhambi, kwa maana nimeisaliti damu isiyo na hatia."*

*... Basi Yuda akavitupa vile vipande vya fedha ndani ya Hekalu akaondoka akaenda kujinyonga. Wale viongozi wa makuhani wakazichukua zile fedha wakasema, "Si halali kuchanganya fedha hizi na sadaka kwa sababu hizi ni fedha zenye damu." Kwa hiyo baada ya kushauriana, waliamua kuzitumia kununulia shamba la mfinyanzi, liwe mahali pa kuzikia wageni. Hii ndiyo sababu lile shamba likaitwa Shamba la Damu hadi leo.* (Mathayo 27:3-4,6-8)

**Unabii wa kuteswa na kufa kwa Yesu msalabani - mwaka wa 700 KK:**

*... hakuwa na chochote katika sura yake cha kutufanya tumtamani. Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulidhania kuwa amepigwa na Mungu, akapigwa sana naye, na kuteswa.*

*Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu; adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.*

*Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, naye Bwana aliweka juu yake maovu yetu sisi sote.*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 20 01-11-2021 20:29:38

*Alionewa na kuteswa, hata hivyo hakufungua kinywa chake; aliongozwa kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya wao wamkataye manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake.*

*Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa. Nani awezaye kueleza kuhusu kizazi chake? Kwa maana alikatiliwa mbali na nchi ya walio hai, alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu. Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu* [alisulibiwa akiwa katikati ya wahalifu wawili], *pamoja na matajiri katika kifo chake* [alizikwa kwenye kaburi la tajiri], *ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*

*Lakini yalikuwa ni mapenzi ya BWANA kumchubua na kumsababisha ateseke. Ingawa BWANA amefanya maisha yake kuwa sadaka* [dhabihu] *ya hatia, ataona uzao wake na kuishi siku nyingi, nayo mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake.*

*Baada ya maumivu ya nafsi yake, ataona nuru ya uzima na kuridhika; kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki, naye atayachukua maovu yao. Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu, naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu, kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti, naye alihesabiwa pamoja na wakosaji. Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji.* (Isaya 53:2-53)

**Mwaka wa l000 KK:**

*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Kwa nini uko mbali hivyo kuniokoa? Mbali hivyo na maneno ya kuugua kwangu?*

*Wote wanionao hunidhihaki, hunivurumishia matusi, wakitikisa vichwa vyao: Husema, "Anamtegemea BWANA, ... Hata hivyo ulinitoa tumboni, ukanifanya nikutegemee, hata nilipokuwa ninanyonya matiti ya mama yangu."*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 21 01-11-2021 20:29:38

*Simba wangurumao wanaorarua mawindo yao hupanua vinywa vyao dhidi yangu. Nimemiminwa kama maji, mifupa yangu yote imetoka katika viungo vyake. Moyo wangu umegeuka kuwa nta, umeyeyuka ndani yangu.*

*Nguvu zangu zimekauka kama kigae, ulimi wangu umegandamana na kaakaa la kinywa changu, kwa sababu umenilaza katika mavumbi ya kifo. Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira, wametoboa mikono yangu na miguu yangu. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote, watu wananikodolea macho na kunisimanga. Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura.* (Zaburi 22:1, 7-9, 13-18)

Kutimia**:**

*Yesu akajibu, "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, wafuasi wangu wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini kama ilivyo, ufalme wangu hautoki hapa ulimwenguni."*

*Pilato akamuuliza, "Kwa hiyo wewe ni mfalme?" Yesu akajibu, "Wewe wasema kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili nilizaliwa, na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Mtu yeyote aliye wa kweli husikia sauti yangu."*

*Pilato akamuuliza Yesu, "Kweli ni nini?" Baada ya kusema haya Pilato akaenda nje tena akawaambia wale viongozi wa Wayahudi waliomshtaki Yesu, "Sioni kosa lolote alilotenda mtu huyu. Lakini ninyi mna desturi yenu kwamba wakati wa Pasaka nimwachie huru mfungwa mmoja mnayemtaka. Je, mnataka niwafungulie huyu 'Mfalme wa Wayahudi'?"*

*Wao wakapiga kelele wakisema, "Si huyu mtu, bali tufungulie Baraba!" Yule Baraba alikuwa mnyang'anyi.*

*Ndipo Pilato akamtoa Yesu akaamuru apigwe mijeledi. Askari wakasokota taji ya miiba, wakamvika Yesu kichwani. Wakamvalisha joho la zambarau. Wakawa wanapanda*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 22 01-11-2021 20:29:38

*pale alipo tena na tena, wakisema, "Salamu! Mfalme wa Wayahudi!" Huku wakimpiga makofi usoni.*

*Pilato akatoka tena nje akawaambia wale waliokusanyika, "Tazameni, namkabidhi Yesu kwenu kuwajulisha kwamba mimi sikumwona ana hatia." Kwa hiyo Yesu akatoka nje akiwa amevaa ile taji ya miiba na lile vazi la zambarau. Pilato akawaambia, "Tazameni, huyu hapa huyo mtu!"*

*Wale viongozi wa makuhani na maafisa walipomwona, wakapiga kelele wakisema, "Msulubishe! Msulubishe!"*

*Pilato akawaambia, "Mchukueni ninyi mkamsulubishe, mimi sioni hatia juu yake."*

*Wayahudi wakamjibu, "Sisi tunayo sheria na kutokana na sheria hiyo, hana budi kufa kwa sababu yeye alijiita Mwana wa Mungu."*

*Pilato aliposikia haya, akaogopa zaidi. Akaingia tena ndani ya jumba la kifalme, akamuuliza Yesu, "Wewe umetoka wapi?" Lakini Yesu hakumjibu. Pilato akamwambia, "Wewe unakataa kuongea na mimi? Hujui ya kuwa nina mamlaka ya kukuachia huru au kukusulubisha?"*

*Ndipo Yesu akamwambia, "Wewe hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu kama hungepewa kutoka juu. Kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako ana hatia ya dhambi iliyo kubwa zaidi."*

*Tangu wakati huo, Pilato akajitahidi kutafuta njia ya kumfungua Yesu, lakini Wayahudi wakazidi kupiga kelele wakisema, "Ukimwachia huyu mtu, wewe si rafiki wa Kaisari. Mtu yeyote anayedai kuwa mfalme anampinga Kaisari."*

*Pilato aliposikia maneno haya akamtoa Yesu nje tena akaketi katika kiti chake cha hukumu, mahali palipoitwa Sakafu ya Jiwe, kwa Kiebrania paliitwa Gabatha. Basi ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka, yapata kama saa sita hivi.*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 23 01-11-2021 20:29:38

*Pilato akawaambia Wayahudi, "Huyu hapa mfalme wenu!" Wao wakapiga kelele, "Mwondoe! Mwondoe! Msulubishe!"*

*Pilato akawauliza, "Je, nimsulubishe mfalme wenu?" Wale viongozi wa makuhani wakamjibu, "Sisi hatuna mfalme mwingine ila Kaisari."*

*Ndipo Pilato akamkabidhi Yesu kwao ili wamsulubishe.*

*Kwa hiyo askari wakamchukua Yesu. Yesu, akiwa ameubeba msalaba wake, akatoka kuelekea mahali palipoitwa Fuvu la Kichwa (kwa Kiebrania ni Golgotha). Hapo ndipo walipomsulubisha. Pamoja naye walisulubisha watu wengine wawili, mmoja kila upande wake, naye Yesu katikati.*

*Pilato akaamuru tangazo liandikwe na liwekwe juu kwenye msalaba wa Yesu, likasema: "YESU WA NAZARETI, MFALME WA WAYAHUDI." Kwa kuwa mahali hapo Yesu aliposulubiwa palikuwa karibu na mjini, Wayahudi wengi walisoma maandishi haya yaliyokuwa yameandikwa kwa lugha za Kiebrania, Kiyunani na Kilatini. Viongozi wa makuhani wa Wayahudi wakapinga, wakamwambia Pilato, "Usiandike 'Mfalme wa Wayahudi,' bali andika kwamba mtu huyu alisema yeye ni mfalme wa Wayahudi." Pilato akawajibu, "Nilichokwisha kuandika, nimeandika!"*

*Askari walipokwisha kumsulubisha Yesu, walichukua nguo zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi lake kwa maana lilikuwa halina mshono bali limefumwa tangu juu hadi chini. Wakaambiana, "Tusilichane ila tulipigie kura ili kuamua ni nani atalichukua."*

*Hili lilitukia ili Maandiko yapate kutimizwa yale yaliyosema, "Wanagawana nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura."*

*Hayo ndiyo waliyoyafanya wale askari.*

*Wakati huo huo karibu na msalaba wa Yesu walikuwa wamesimama mama yake, na dada wa mamaye, na Maria*



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 24 01-11-2021 20:29:39

*mke wa Klopa, na Maria Magdalene. Yesu alipomwona mama yake mahali pale pamoja na yule mwanafunzi aliyempenda wamesimama karibu, akamwambia mama yake, "Mwanamke, huyo hapo ndiye mwanao," Kisha akamwambia yule mwanafunzi, "Nawe huyo hapo ndiye mama yako." Tangu wakati huo yule mwanafunzi akamchukua mama yake Yesu nyumbani kwake.*

*Baada ya haya, Yesu hali akijua kuwa mambo yote yamemalizika, alisema ili kutimiza Maandiko, "Naona kiu." Hapo palikuwa na bakuli lililojaa siki. Kwa hiyo wakachovya sifongo kwenye hiyo siki, wakaiweka kwenye ufito wa mti wa hisopo, wakampelekea mdomoni. Baada ya kuionja hiyo siki, Yesu akasema, "Imekwisha." Akainamisha kichwa chake, akaitoa roho yake.*

*Kwa kuwa ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka, Wayahudi hawakutaka miili ibaki msalabani siku ya Sabato, hasa kwa kuwa hiyo Sabato ingekuwa Sikukuu. Wakamwomba Pilato aamuru miguu ya wale waliosulubiwa ivunjwe ili wafe haraka miili iondolewe kwenye misalaba. Kwa hiyo askari wakaenda wakavunja miguu ya mtu wa kwanza aliyesulubiwa pamoja na Yesu na yule mwingine pia. 3Lakini walipomkaribia Yesu, wakaona ya kuwa amekwisha kufa, hivyo hawakuvunja miguu yake. Badala yake mmoja wa wale askari akamchoma mkuki ubavuni na mara pakatoka damu na maji. Mtu aliyeona mambo hayo ndiye alitoa ushuhuda, nao ushuhuda wake ni kweli. Anajua kuwa anasema kweli, naye anashuhudia ili pia nanyi mpate kuamini. Kwa maana mambo haya yalitukia ili Maandiko yapate kutimia, yale yasemayo, "Hakuna hata mfupa wake mmoja utakaovunjwa." Tena Andiko lingine lasema, "Watamtazama yeye waliyemchoma."*

(Yohana 18:36-19:37)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 25 01-11-2021 20:29:39

**Unabii wa Kufufuka kwa Yesu - mwaka wa 1000 KK:**

*Nimemweka* B*WANA* *mbele yangu daima. Kwa sababu yuko mkono wangu wa kuume, sitatikisika. Kwa hiyo moyo wangu unafurahia, na ulimi wangu unashangilia; mwili wangu nao utapumzika salama, kwa maana hutaniacha kaburini, wala hutamwacha Mtakatifu Wako kuona uharibifu.* (Zaburi 16:8-10)

**Kutimia:**

*Mnamo siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema, wale wanawake walichukua yale manukato waliyokuwa wameyaandaa, wakaenda kaburini. Wakakuta lile jiwe limevingirishwa kutoka kwenye kaburi, lakini walipoingia ndani, hawakuuona mwili wa Bwana Yesu. Walipokuwa wanashangaa juu ya jambo hili, ghafula watu wawili waliokuwa wamevaa mavazi yanayong'aa kama umeme wakasimama karibu nao. Wale wanawake, wakiwa na hofu, wakainamisha nyuso zao mpaka chini. Lakini wale watu wakawaambia, "Kwa nini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa wafu? Hayuko hapa; amefufuka! Kumbukeni alivyowaambia alipokuwa bado yuko pamoja nanyi huko Galilaya kwamba: 'Ilikuwa lazima Mwana wa Adamu atiwe mikononi mwa watu wenye dhambi na waovu ili asulubiwe, na siku ya tatu afufuke.' " Ndipo wakayakumbuka maneno ya Yesu.*

*Waliporudi kutoka huko kaburini, wakawaeleza wale wanafunzi kumi na mmoja pamoja na wengine wote mambo haya yote. Basi Maria Magdalene, Yoana, na Maria mama yake Yakobo, pamoja na wanawake wengine waliofuatana nao ndio waliwaelezea mitume habari hizi. Lakini hawakuwasadiki hao wanawake, kwa sababu maneno yao yalionekana kama upuzi.* (Luka 24:1-11)

**Unabii wa Yesu Kupaa Mbinguni - mwaka wa 1000 KK:**

B*WANA* *amwambia Bwana wangu: "Keti mkono wangu wa kuume, mpaka nitakapowafanya adui zako kuwa mahali pa kuweka miguu yako."* (Zaburi 110:1)



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 26 01-11-2021 20:29:39

Kutimia**:**

*Mitume walipokuwa wamekusanyika pamoja, wakamuuliza Yesu, "Bwana, je, huu ndio wakati wa kuwarudishia Israeli ufalme?" Yesu akawaambia, "Si juu yenu kujua nyakati na majira ambayo Baba ameyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia."*

*Baada ya kusema mambo haya, walipokuwa wanatazama, akachukuliwa juu mbinguni mbele ya macho yao na wingu likampokea wasimwone tena.*

*Walipokuwa bado wakikaza macho yao kuelekea juu alipokuwa akienda zake Mbinguni, tazama ghafula, wanaume wawili waliovaa mavazi meupe wakasimama karibu nao, wakasema, "Enyi watu wa Galilaya, mbona mnasimama mkitazama juu angani? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda Mbinguni, atarudi tena jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake Mbinguni."*
(Matendo 1:6-11)

**Unabii wa Israeli kutubu na kumrudia Yesu ambao haujatimia - mwaka wa 480 KK:**

*"Nami nitamiminia nyumba ya Daudi na wakazi wa Yerusalemu roho ya neema na maombi. Watanitazama mimi, yule waliyemchoma. Nao watamwombolezea kama mtu anayemwombolezea mwanawe wa pekee na kusikitika kwa uchungu kama anayemsikitikia mzaliwa wake wa kwanza wa kiume."* (Zekaria 12: 10)

**Unabii wa hali yetu sasa ambapo watu hupenda kumtenganisha Yesu Mwana na Mungu Baba - mwaka wa 1000 KK:**

*Wafalme wa dunia wanajipanga na watawala wanajikusanya pamoja dhidi ya Bwana na dhidi ya Mpakwa Mafuta wake* [Mpakwa Mafuta yaani Masihi au



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 27 01-11-2021 20:29:39

> Kristo]. *Wanasema, "Tuvunje minyororo yao na kuvitupilia mbali vifungo vyao."*
>
> *... Nitatangaza amri ya Bwana: Yeye aliniambia, "Wewe ni Mwanangu, leo mimi nimekuzaa* [lakini tafadhali uelewe: si kuzaa kimwili]. Niombe, nami nitayafanya mataifa kuwa urithi wako, miisho ya dunia kuwa milki yako."
>
> (Zaburi 2:2-3, 7-8)

**Yesu Mwenyewe alinena:**

> *"... Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi."*
>
> (Mathayo 20:28)

> *"Hii ndiyo damu yangu ya Agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi."* (Mathayo 26:28)

> *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*
>
> (Yohana 3:16)

> *"... Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo ... nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo ... Hakuna mtu aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa kwa hiari yangu mwenyewe ..."* (Yohana 10:11, 15, 18)

**Hakuna mwanadamu anayeweza kuitangua asili yake ya dhambi kwa juhudi yake ya kutenda mema**

Hakuna mkosoaji duniani anayeweza kuuelezea vinginevyo ushahidi wa unabii huu mwingi uliotimia. Ni wa kipekee katika historia yote na kwenye vitabu vyote vya dini. Ni muhuri wa Mungu uliofumana na ujumbe wake kwa wanadamu ili mtafutaji ye yote mnyenyekevu na mwaminifu aweze kuhakikishiwa kikamilifu kuwa hasomi tu vitabu vya hadithi vilivyotungwa na baadhi ya watu wa kidini wanaojaribu kuonyesha mitazamo yao kwa



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 28 01-11-2021 20:29:39

wengine. Kwenye ushahidi uliotolewa hakuna anayeweza kudai kuwa Biblia imepotoshwa!

Basi huenda Agano la Kale, angalau kwa sehemu, liliandikwa baada ya Agano Jipya ili "litoe unabii" kama huo? Hili halifikiriki kwa sababu kadhaa. Wayahudi waliyalinda Maandiko kwa hadhari na uangalifu wa hali ya juu kabisa. Wao wenyewe kwa kweli hawakupenda kuwa na unabii huu kwenye Kitabu chao Kitakatifu, maana unapingana na imani na desturi zao wenyewe. Ina maana kwamba vifungu hivi kamwe havisomwi kwenye usomaji wa kila mara wa siku ya Sabato kwenye Sinagogi lo lote. Lakini pamoja na hayo Agano la Kale tayari lilikuwa limeenea kabla ya kuja Kristo na lilikuwa limetafsiriwa katika Kigiriki kati ya mwaka wa 300 na 200 KK. Hivyo haiwezekani kabisa 'kupitia upya' andiko lililoenea. Na zaidi, tunazo nakala za Agano la Kale la kabla ya Ukristo zenye unabii huu.

## HITIMISHO

Umekuwa na ujasiri wa kulinganisha! Sasa ni wakati wa kufikia uamuzi wako mwenyewe. Utakuwa umegundwa:

1. Ushahidi wa walioyaona kwa macho yao, na wa wanahistoria, na wa unabii uliotimia, hauwezi kufutiliwa mbali kwa sababu tu haukubaliani na dhana au matarajio ya mtu fulani.
2. Kupotoshwa kwa Biblia kunakodaiwa ni kashfa yenye nia mbaya inayoitafsiri vibaya Biblia na Kurani. Msingi wake ni fikira potovu na makosa madogo ya kunakili nje ya uwiano. Kama Kurani inaweza kufanyiwa uchunguzi makini ule ule, itakuwa dhahiri kama ilivyo kwenye Biblia kuwa mahali fulani mkono wa mtu uliingilia.
3. Ushahidi wote huo huunga mkono ukweli kuwa Yesu Kristo yuko vile anavyodai kuwa katika Biblia: Kuwa yeye ndiye njia ya pekee ya Mungu ya kumwezesha mwanadamu kukombolewa kutoka kwenye maangamizi ya milele yanayotisha, ambayo ni matokeo ya kushindwa kwake wakati wote kufanya mapenzi ya Mungu. Kwa

namna yetu yenye ubinafsi ya kufikiri na kutenda, wote tumeshindwa kuutii mpango wa Mungu kwa maisha yetu. Hivyo wanadamu wote tumekuwa wenye dhambi. Wote tunahitaji msamaha ili tuweze kuingia kwenye uwepo wa Mungu katika utukufu. Hakuna mtu anayeweza kujitakasa mwenyewe.

- Hakuna mwanadamu awezaye kuitangua asili yake ya dhambi kwa kujitahidi kuwa mwema.
- Hakuna mwanadamu anayeweza kusamehewa bila ya kuiomba karama ya Mungu ambayo hakuistahili: Radhi ya Mungu.
- Kulingana na Torati na Injili msamaha huu hautatolewa bila ya adhabu hiyo kuitekeleza kwa Yesu.
- Yesu ndiye njia pekee ya kuturudisha kwa Mungu. Ndiye tumaini letu pekee la uzima wa milele.
- Hakuna aliye na hisia na upendo wa kawaida kwa Mungu atakayeyapuuza madai haya asiyachunguze kwa makini huku akiuzingatia ushahidi wake wote.
- Hakuna kukataliwa au kuteswa na watu kunakoweza kututisha tuikatae kweli ya Mungu, radhi yake, msamaha wake na karama yake ya uzima wa milele kama ilivyoshuhudiwa!



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 30 01-11-2021 20:29:39

**Mpendwa msomaji,**

Umefikia uamuzi gani baada ya kusoma kijitabu hiki? Tafadhali tujulishe.

Tunaahidi nakala nyingine ya bure ya moja ya machapisho yetu ukitupa majibu.

1. Wewe kama Mwislamu, umewahi kulinganisha mafundisho ya Biblia na Kurani?
2. Kulingana na Surah al-Ankabut 29:46 mtazamo wa Mwislamu kwa Wakristo unapaswa uwe aje?
3. Kwa nini Mkristo ye yote wa kweli hapaswi kamwe kuongeza wala kupunguza lo lote kwenye Biblia?
4. Tupe maoni yako kuhusu Ibn-Khazm alivyochukulia kupingana kati ya Kurani na Injili.
5. Ni zipi baadhi ya sifa alizopewa Yesu katika Kurani?
6. Unaweza kutupa maana halisi ya neno la Kiswahili ‘Yesu’?
7. Taja majina ya mashahidi watatu au zaidi walioona maisha, kufa na kufufuka na kupaa mbinguni kwa Yesu.
8. Elezea umuhimu wa 2 Petro 1:16-21.
9. Mwanahistoria wa Kiyahudi Josephus alisemaje kuhusu Yesu?
10. Umevutiwa zaidi na upi kati ya unabii mwingi uliotimizwa kuhusu Yesu, na kwa nini?
11. Kwa nini haifikiriki kuwa Agano la Kale au sehemu yake ingeweza kuandikwa baada ya vitabu vya Agano Jipya?
12. Ni nini uamuzi wako kuhusu Yesu Kristo?

Tafadhali tutumie majibu yako pamoja na maswali au masuala yo yote unayopenda kujadili.

Asante.



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 31 01-11-2021 20:29:39

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo wako

Al-Kitab - *Kitabu cha Vitabu* (Kozi ya Biblia)

*Tafadhali nitumie* ....................................................................

.............................................................................................

.............................................................................................

.............................................................................................

Tuma barua yako kwa:

**Hamasa ya Milele**
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

**Life Challenge**
S.L.P. Box 50770- 00200
Nairobi, KENYA
info@lifechallenge.de



02DareToCompare-Swahili -Edited by SB.indd 32 01-11-2021 20:29:39